**Ewald Frank**

## Myaka Makumi Sita Kukazi Ya BWANA

Nina salimu wandugu wote na wadada salamu kutoka kilindi cha moyo katika jina la BWANA wetu Yesu Kristo. Nilichaguwa neno la mutume Paulo; kama neno la kuanza, yeye aliyekuwa amepokeya utume wa hapohapo na kuwekwa katika utumishi, 1 Timotheo 1:12:

*"Nami namshukuru Kristo Yesu BWANA wetu, aliyenitia nguvu kwa sababu aliniona kuwa mwaminifu akaniweka katika utumishi wake…"*

Kama vile munavyo juwa nyinyi nyote, nimetakasiya maisha yangu kwa BWANA kwa mwaka ya 1949, katika mukutano wa kipentekosti huko Hambourg. Na kwa hio muda ndipo nilisikiya mara yakwanza kusema kuhusu utumishi wakipekee ya ndugu Branham. Kwa mwaka wa 1955 nilipata heri ya kushiriki mikutano ambayo alikuwa imetayarishwa huko Karisruhe/Ujerumani na kuweza kumujuwa kwa kipekee kwa mazungumu yangu naye ya kwanza.

Baada ya myaka 60, nikonasema mara moja tena kwa kitendo cha ajabu cha siku ya kwanza tarehe 2, Aprili 1962. Nisasema kweli mbele ya Mungu. Hiyo ilinifikia mbele ya jua kutokea: kutoka upande wa kuume kwa dirisha, BWANA akasema maneno haya: **"Mutumishi wangu, muda wako katika muji huu inakaribia kwisha. Nitakutuma katika miji mingine kwa kuhubiri neno langu."** Nilinyanyuwa mikono yangu na kusema: "BWANA, hawata nisikia…" BWANA akajibu **"Mutumishi wangu, wakati itakuja ambapo watakusikia. Weka chakula kwenye galani, kwani njaa kubwa inakuja. Na hapo utasimama katika ya taifa utagawa chakula…"**

Kwa mwezi ya disemba 1962 nilienda kutembelea ndugu Branham huko Jeffersonville, kupitia ufunuo wa kiungu aka rudiliya neno kwa neno kwa kingereza, yale ambayo BWANA alikuwa ame niagiza katika kijerumani tarehe 2, Aprili. Wandugu Fred Sothman na Banks Wood walikuwa hapo tayari wale ni washuhunda wa hiyo. Ndipo sasa ndugu Branham akanitafsiria: "Chakula ambacho uta weka kwa gala, si chakula ya mwili, kama vile ulivyo waziya, ila ni Neno lililoahidiwa kwa wakati huu, lililo katika ma-

hubiri yaliyo wekwa kwenye kanda. Lakini ngoja mbele ya kuanza ugawaji mpaka utakapo pokea yaliyo baki ambayo ni moja ya hiyo.”

Tunajuwa sisi wote ya kwamba ndugu Branham, nabii aliyeahidiwa (Malaki 4:5) tarehe 11, Juni 1933: **“Kama vile yohana mbatizaji alivyo tumwa kama mtangulizi wa kuja kwa kwanza kwa Kristo, Hivyo utatumwa na ujumbe ambao utatangulia kuja kwa pili kwa Kristo”.** Yeye mwenyewe amerudilia maneno hayo maranyingi: “siyo mimi, lakini ujumbe utatangulia, kuja kwa pili kwa Kristo”. Mungu alimtumikisha,ili afunuwe masiri zote na kuweka chakula cha kiroho. Tarehe 11 Juni 1958 huko Dallas Texas, aliniambia kwa mwisho ya mazungumuzo yetu: “Ndugu Frank, utarudi ujerumani na ujumbe huu”. Tangu wakati ule, mahubiri yake yote yaliyo kuwa kwenye kanda tulianza yitumiwa kwa kawaida na nilianza kuzitafsiri.

Na ginsi ni kweli, ginsi BWANA alinipa utume, niliyitumika kwa namna mbali mbali. Baada ya kifo cha ndugu Branham nilitanganza Neno la Mungu Duniani pote. Katika safari zangu za kupasha injili, nilikuwa niki hubiri mara pili ao mara tatu katika muji mmoja na kisha hapo ni naenda kwa muji yengine.

Na makanisa za pahali ziliundwa na wandugu wanaokaa mahali pale.

Tarehe 2 Aprili 1962, ndiyo siku ambayo BWANa alinipa utume na kuniweka kwa kazi yake. Katika hiyi myaka 60, alinipa maagizo yake kupitia sauti yake kuhusiana na hudma yangu. Nina shuhudiya ya kwamba hiyo haikufanyika kwa ndoto,ila kila wakati nilipokuwa ni kiwa macho. Nina weza kusema siku, na pahali, na saa ya kila wakati. Nani hivi BWANA alinisemesha kwa hii siku ya 19, septemba, 1976 huko Edmonton, siku ya juma pili asubui, na sauti ya sheriya: **“Mutumishi wangu, ni mekuweka, kulingana na Mathayo 24:45-47, kwa ugawaji wa chakula kwa wakati unao faa”.** Yeyeyote anayewezakusoma andiko hii atakuta shahili ya 47 inasema “*… ata (BWANA) muweka juu ya vitu vyote vyake”.* Kwa wakati wetu shahururi zote za Mungu zimefunuliwa kuliko siku za mbele. Kama Paulo na mimi na weza pia kushuhudia: *“kwa maana sikujiepusha na kuwa hubiri habari ya kusudi lote la Mun-*

*gu"* (Matendo 20:27). Kila somo la Biblia lilipata dawa kupitia mahubiri yangu, vitabu, brocha,na baruwa za mzunguko.

Katika mathayo 24, BWANA wetu hakutabiri tu kuhusu kubomolewa kwa hekalu, kusambazwa kwa taifa la Israeli na kurudi katika inchi yao, katika hadisi ya mtini (shahili 32); alitabiri pia kuhusu yale ambayo yatatimia kwa wakati wa mwisho, kuhusu vita, njala, na matetesi ya vita na tetemeko za nchi na nyakati za hatari. Humo kuko pia shahili ya 14: *"Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote kuwa ushuhuda kwa mataifa yote, hapo ndipo ule mwisho utakuja"*. Kama vile inavyo andikwa kwa shahili la 45 mpaka 47, nikusema wazi wazi kwa utangazaji wa Neno na ugawaji wa chakula cha kiroho.

Tunaishi kwa kweli tena katika siku za kibiblia, ambamo BWANA mwenyewe ametuma mtumishi wake na nabii pamoja ujumbe na alinipa agizo la kuhubiri Neno lililofunuliwa na kugawa chakula kilicho wekwa kwenye gala- mana iliyofichwa. Hudma ambayo BWANA amenipa inafungwa kwa hudma ya ndugu Branham hapo hapo kama vile utumishi wa Yosuwa ulikuwa ukiambatana na utumishi wa Musa. Musa alitowa taifa katika utumwa kama vile BWANA alivyo kuwa ameahidi Ibrahimu katika Mwanzo 15:13, na Yosuwa aliigiza taifa katika inchi ya Ahadi (wagalatia 4:28) na tunaami ni yale yanayo andikwa katika 2 wakorintho 1:20: *"Maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika yeye ni ndiyo; tena kwa hiyo katika yeye ni Amina; Mungu apate kutukuziwa kwa sisi"*. Tuna amini kila ahadi ambayo Mungu ametupatiya ndani ya Neno na tutaziona na kuziishi katika utimilifu wake.

Muniache niseme wazi wazi: haiko kuhusu ndugu Branham ao ndugu Frank, bali ni maahadi za Neno la wakati huu. Ni Mungu mwenyewe, anaye amuwa ni nani ambae atamchaguwa ili atimize kazi fulani ya kipekee na sababu mkubwa, ikiwa kuna swali ya mwito ambayo inaambatana na mpango wa okovu wa Mungu. Paulo hakuomba ili apokee mwito, ndugu Branham hakuomba iliapokee mwito;nami sikuomba kusudi ni pate mwito. Lakini Mungu alikuwa ametayarisha hiyo katika umilele, na hivyo ndivyo alivyo timia kwa wakati yetu. Alichosema BWANA wetu bado kinatumika: *"Kweli kweli na waa mbieni Yule amaempokea yeye ambae nina mtuma amenipokea mimi, nayeyeanae nipokea mimi anampokea Yule alie*

*nituma* (Yohana 13:20). Yeye anae pita kinyume ya yaleambayo Mungu anayo fanya kulingana na Neno lake anapita pembeni ya Mungu, kama vile madhehebu mengine na anajenga ufalme wake mwenyewe.

Kwa mwaka 1962, nilikuwa nikifikisha myaka 29, tangu Mungu alipo nituma, sasa nina fikia karibu myaka 89 na niliona myuma,kwa shukrani, kwa myaka hii yote iliyo pita kwazi yake. Sitoe ushuhuda wangu mwenyewe, ni natowa ushuhuda pekee yake mbele ya Mungu mkubwa kwa yale ambayo ya nasehemu kwa mwito na kwa yale yote ambayo BWANA alifanya katika ma inchi zote za dunia mzima. Ujumbe wa milele wa okovu inafungwa ndani mafundisho yote ya kibiblia na ilitangazwa duniani pote. BWANA anasema: *"… Hapo ndipo mwisho uta kuja"*. Sisi tunayo amini ujumbe wa mwisho wa wakati tunaweza kushuhudia kwamba Mungu ametufunulia siri zote za neno ya mpango wa okovu na amerudisha vyote.

Nina waomba kusoma kwa makini andiko ifwatayo inayo tembe na hudma/utumishi yangu:

*"Ni kuhusu (Kanisa) ambalo nimefanywa mhudumu wake, sawa sawa na uwakili wa Mungu, niliopewa kwa faida yenu nilitimize Neno la Mungu; siri ile ilifichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake, ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hili katika mataifa, nao ni Kristo ndani yenu tumaini la utukufu"* (Wakolosai 1:25-27).

Mungu alifanya kwa namna yote neema kwa safari za utangazaji wa injili katika hii myaka yote, mawasiliano ziliwekwa Duniani pote,na sasa kwa kusambaza kwa mtandao mahubiri kwa lugha zote, waamini wa kweli wote wana weza kusikia ile ambayo roho anaambia Kanisa, na inarihusu Kanisa lake kurudi kwa hatuwa moja pamoja na Neno lake, kama vile ilivyo kuwa mwanzoni.

Mikutano ya Dunia mzima hapa kwenye kituo cha misheni cha Krefeld, haita weza fanyika tena kama vile ilivyo kuwa ikifanyika kwa myaka 40. Vile vile sitafanya tena safari za kimishonary. Sasa waamini wote wana kusanyika kila mahali ambapo inawezekana kwa kuomba na kusikia mahubiri na fasi yoyote abapo wako

watashiriki kwa yale ambayo Mungu atafanya kwa ajili ya kumaliza kazi yake.

Tunashukuru BWANA kwa ajili ya wandugu wanayo tayarisha na kusambaza mahubiri kwa mtandao na pia wandugu wanao tafsiri kwa lugha mbali mbali na pia kwa wandugu wote wanao tumika katika hudma wanaoleta ile Neno moja moja, chakula safi chakiroho kwa taifa la Mungu Duniani pote. "*Mutu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo kinywani mwa Mungu*"(Mathayo 4:4). Inaomba sasa wale wote wanayo unda Kanisa bibi-arusi waongozwe katika upendo wa Mungu kupitiya Roho Mtakatifu, kwa umoja wa kiungu, ili kila mmoja aweze kufikia umoja wa kipekee pamoja na Mungu na kuishi matayarisho ya kepekee na mazoezi ya okovu kama vile mwanzoni na kungojea unyakuo, tukiambatana na Neno la Mungu.

Ndugu Branham alifanya sehemu yake, nami nimefanya sehemu yangu. BWANA mwenyewe atamaliza kazi yake ya ukombozi kwa nguvu na kitendo cha roho mtutakatifu ndani ya Kanisa bibi-arusi ili lipate kuwa tayari kwenda kumulaki Bwana arusi (Mathayo 25:10, 1 Wathesalonike 4:15-18, 1 Wakoritho 15:51-58).

Tunaona maandiko ya wakati huu ikimiya machoni petu, na tuna weza kuinuwa vichwa vyetu kwa kuwa ukombozi wa myili yetu ni karibu.

"*Na roho na bibi arusi wasema njoo! Naye asikiaye na aseme njoo!…*"(Ufunuo 22:17a). "*Amina! Njoo Bwana yesu!*"

Inafanyika kwa upande wa Mungu.

EWALD FRANK